



**BARAZA LA KIPAPA LA MAJADILIANO YA KIDINI**

**UJUMBE KWA AJILI YA MWISHO WA RAMADHANI**  
**'Id al-Fitri 1432 H. / 2011 A.D.**

***Wakristo na Waislam:***  
***Kufanya kazi pamoja kwa ajili ya Ukuu wa Kiroho wa mwanadamu***

**Vatican City**

Wapendwa Marafiki Waislam,

1. Mwisho wa mwezi wa Ramadhani unaipa Halmashauri ya Kipapa ya Mazungumzano na Dini mbalimbali fursa nzuri ya kuwaletea kwa moyo wa dhati salamu zetu tukitumaini kwamba juhudi mlizozifanya kwa ukarimu wakati wa mwezi huu zitaleta matunda yote ya kiroho yaliyotamaniwa.

2. Mwaka huu tumefikiri tuipe kipaumbele damira ya *Ukuu wa Kiroho wa nafsi ya mwanadamu*. Hii inahusu ukweli ambao Wakristo na Waislam wanafikiri kuwa ina umuhimu wa kwanza, wanapokabiliwa na changamoto za uyakinifu na malimwengu. Uhusiano ambao kila mwanadamu anao juu ya kile kinachopita uwezo wa mtu si wa muda tu katika historia, bali ni sehemu ya hulka ya binadamu. Hatuamini katika majaliwa, tunaridhika-zaidi ya hayo ni mang'amuzi yetu-kwamba Mungu anatuongoza katika mapito yetu.

3. Wakristo na Waislam, licha ya tofauti zao, wanatambua hadhi ya mwanadamu aliyejaliwa haki na wajibu. Wanafikiri kwamba, akili na uhuru ni mapaji kweli ambayo yanatakiwa kuchochea waumini kutambua tunu hizi ambazo zinagawanywa kwa sababu zinakaa katika asili ileile ya mwanadamu.

4. Hii ndiyo sababu upelekaji wa tunu kama hizo za kibinadamu na kimaadili kwa vizazi vipya unakuwa ni wajibu wa wote. Ni wajibu wetu kuwasaidia kugundua kwamba kuna wema na ubaya, kwamba dhamiri ni kitu kitakatifu kinachotakiwa kuheshimiwa, na kwamba kuunda ukuu wa kiroho unatufanya tuwe wawajibivu zaidi, wasidivu zaidi, wanaokuwa tayari zaidi, kwa ajili ya manufaa ya wote.

5. Wakristo na Waislam mara nyingi mno wanakuwa mashahidi wa mashambulizi dhidi ya kile kitakatifu, kwa lengo la kutokuwaamini wale wanaojiita waumini. Tutashindwa kutoikataa miundo yote ya ung`anganizi na vitisho, chuki bila sababu na tuhuma za mijadala na pia ubaguzi ambao, mara nyingine, waumini ndio walengwa katika maisha ya kijamii na kisiasa na kadhalika katika vyombo vya habari.

6. Tuko karibu nanyi sana kiroho, Marafiki wapendwa, tukimwomba Mungu awape nguvu mpya kiroho na tunawaletea matashi yetu ya dhati kwa ajili ya amani na furaha.

Jean-Louis Kardinali Tauran  
*Rais*

Askofu Mkuu Pier Luigi Celata  
*Katibu*

**PONTIFICAL COUNCIL  
FOR INTERRELIGIOUS DIALOGUE**  
00120 Vatican City

Telephone: 0039.06.6988 4321 / 06.6988 3648

Fax: 0039.06.6988 4494

E-mail: [dialogo@interrel.va](mailto:dialogo@interrel.va)

[http://www.vatican.va/roman\\_curia/pontifical\\_councils/interelg/index.htm](http://www.vatican.va/roman_curia/pontifical_councils/interelg/index.htm)